

Mwongozo kwa watu waliopata chanjo kamili



Unachukuliwa kuwa umepata chanjo kamili wiki 2 baada ya dozi yako ya mwisho ya chanjo ya COVID-19.

Chanjo za dozi mbili: Wiki 2 baada ya dozi ya 2 (unahitaji dozi zote mbili ili kuwa salama kikamilifu).

Chanjo ya dozi moja: Wiki 2 baada ya dozi (unahitaji dozi moja tu ili kuwa salama kikamilifu).

Ili kuweka wengine salama hadi watu wengi wapate nafasi ya kupata chanjo, kunaweza kuwa na hali ambapo bado unahitaji kuchukua tahadhari.

Mara baada ya kupata chanjo kamili:



Unaweza kutembelea maeneo ya ndani ya nyumba na kutangamana kwa karibu na watu wengine ambao wamepata chanjo, bila kuwa na wasiwasi kuhusu mtu kuugua.



Unaweza kutembelea mtu ambaye ana hatari ndogo ya kuathiriwa na maradhi makali na ambaye bado hajapata chanjo, bila kuwa barakoa au kuhakikisha umbali wa kimwili.



Sio lazima ujiweke karantini au upimwe ikiwa umetangamana kwa karibu na mtu aliye na COVID-19, isipokuwa kama utapata dalili baada ya kutangamana kwa karibu (hali ambayo itakuwa nadra).




CORONAVIRUS
UTAH.GOV

Ili kuhakikisha usalama kwa wengine hadi watu wengi waweze kupata chanjo:



Vaa barakoa na uhakikishe umbali wa kimwili wakati uko karibu na mtu ambaye bado hajapata chanjo na yuko katika hatari kubwa ya kuathiriwa na maradhi makali au anayeishi na mtu aliye katika hatari kubwa.



Vaa barakoa na uhakikishe umbali wa kimwili katika maeneo ya umma hadi watu wengi wapate nafasi ya kupata chanjo.



Epuka umati na mikusanyiko mikubwa. Vaa barakoa na uweke umbali wa kimwili iwezekanavyo ikiwa uko karibu na watu wengi.



Chanjo za COVID-19 zina ufanisi katika kuzuia maradhi makali, kulazwa hospitalini, na kifo kutokana na virusi. Ikiwa katika hali nadra utapata dalili za COVID-19, unahitaji kupimwa.



Fuata tahadhari zozote ambazo utaombwa kufuata na biashara na waajiri. Huenda wana wafanyakazi au wateja ambao bado hawajapata chanjo, au ambao wako katika hatari kubwa ya kuathiriwa na maradhi makali.



Ikiwa unasafiri, fuata masharti yoyote ya eneo unalosafiri.